JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Anwani ya Simu:"UCHUNGUZI"
Simu Nambari: (027) 2645186
Nukushi: (027) 2647885
Barua Pepe: rbctanga@pccb.go.tz
Tovuti: www.pccb.go.tz

Barabara ya Hospitali ya Bombo,
S.L.P 1953,
21105 TANGA,
TANZANIA.

TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

MEI, 2023

TAKUKURU YAOKOA JUMLA YA SH. 69,506,327.82 ZA USHURU KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA.

Ndugu Waandishi wa Habari,

1. UZUIAJI RUSHWA

TAKUKURU tuna jukumu la Ufuatiliaji wa Uzingativu wa Sheria katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2023, TAKUKURU Tanga katika kutelekeza jukumu hili ilibaini uwepo wa mtoa huduma za uwakala wa makusanyo ya ushuru na maduhuli ya Serikali katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ambaye alikuwa amekusanya ushuru kiasi cha **Tsh. 83,709,953.52 /=** pasipo kuingiza fedha hizo kwenye akaunti ya benki, kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Novemba 2022. Baada ya kubaini hilo, TAKUKURU kwa kushirikiana wa ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, walimtaka Mmiliki wa kampuni ya uwakala wa ushuru kuingiza fedha hizo kwenye akaunti ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza katika Benki ya NMB ndani ya muda wa miezi mitatu kuanzia Januari 2023 hadi Machi 2023**.**

Aidha kufikia tarehe 27.3.2023 tayari jumla ya **Tsh. 69,506,327.82** zilikuwa zimerejeshwa kufuatia wakala huyo kutekeleza agizo la kuingiza fedha hizo za makusanyo ya ushuru kwenye akaunti ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza katika benki ya NMB. Kufikia tarehe 04.05.2023, fedha zilizobakia ni Tsh. 14,203,625.70 ambazo Mpango uliowekwa ni kwamba, fedha zote zinapaswa kuingizwa kwenye Akaunti ifikapo June 2023.

2. UFUATILIAJI WA MIRADI

Ndugu Waandishi wa Habari,

Katika Jukumu la Uzuiaji Rushwa, ili kubaini mianya ya vitendo vya rushwa na kushauri namna bora ya kuweka mifumo madhubuti na imara inayoweza kuchangia katika ufanisi na uwazi, tumefanya kazi ya Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo 70 yenye thamani ya Sh.**41,222,441,015.37 na** Katika ufuatiliaji huo, miradi 18 yenye thamani ya **Sh.** 10,044,396,276.86 ilibainika kuwa na mapungu kama ilinavyoonekana hapa chini.

Jedwali Na. 1: Miradi yevye Mapungufu:

Wilaya	**Jina la Mradi**	**Thamani (TSH)**	**Mapungufu**	**Hatua zilizochukuliwa**
Korogwe	Mikopo ya 10% za makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa makundi maalum (Vijana, Wanawake na watu wenye Ulemavu)	173,508,787.00	-wanasiasa kuingilia mchakato wa utoaji wa mikopo hasa madiwani, - Vikundi kushindwa kutunza taarifa za fedha, - Wanavikundi kugawana fedha ya mikopo badala ya kuifanyia kazi pamoja.	Jalada la Uchunguzi limefunguliwa na Uchunguzi umeanzishwa.
	Ujenzi wa mradi wa maji Chekelei	2,615,582,697.00	Mradi huu ulikuwa na changamoto ya kifedha.	Mamlaka husika (RUWASA) imeshafanya maombi ya fedha kukamilisha mradi
	Ujenzi wa jengo la utawala Halmashauri ya wilaya korogwe.	2,700,000,000.00.	Baadhi ya vifaa vya ujenzi vimenunuliwa kwa bei kubwa kuliko uhalisia na baadhi ya vifaa vya ujenzi vimenunuliwa idadi kubwa kuliko mahitaji	Uchunguzi umekamilika na tayari watuhumiwa wameshafikishwa mahakamani
	Ujenzi wa nyumba	150,000,000.00	mradi huu una changamoto ya Kusitishwa kwa mkataba wa ujenzi	Mchakato wa Kumpata fundi

	ya Mkurugenzi wa Wilaya ya Korogwe		kati ya fundi na Halmashauri jambo ambalo limekwamisha uendelezaji wa Mradi na kupelekea mradi kumesimama	mwingine umesha fanyika.
Mkinga	Mradi wa ujenzi wa shule ya Sekondari Kigongoi Mangaribi	470,000,000/=	-Makampuni yanayo sambaza vifaa vya ujenzi kubainika kuwa si Makampuni ya vifaa vya ujenzi. -Utata wa Masharti yaliyomo kwenye Mkataba. -Kukosekana kwa ushindani baina ya Makampuni yanayo sambaza vifaa vya ujenzi baada ya kubainika kuwa yote yanamilikiwa na mtu mmoja. -Fedha za mradi kuingizwa katika akaunti binafsi ya Mwalimu Mkuu.	-Kufuatilia Taarifa za Usajili na umiliki wa Makampuni tajwa. -Kupata maoni ya Kisheria juu ya Mikataba Masharti yaliyomo kwenye Mikataba..
	Mikopo ya 10% za makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa makundi maalum (Vijana, Wanawake na watu wenye Ulemavu)	343,033,329.37	-Kutolewa kwa Mikopo kwa fedha chache tofauti na fedha zilizotengwa. -Baadhii ya Vikundi havikurejesha fedha.	DED ametaarifiwa afanye ukaguzi/ufuatiliaji wa fedha ambazo hazikukopeshwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 hadi 2022/2023 ili kujua fedha hizo zimetumika wapi.

kilindi	Mikopo ya 10% za makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa makundi maalum	**252,577,273**	katika marejesho, bodo kuna marejesho mengi hayajafanywa na vikundi nufaika **kwa mwaka 2021/2022 na 2022/2023** zilikopeshwa kiasi cha Tsh **91,309,236** hakijarejeshwa kwa makundi yote matatu	ufutiliaji umeanza kwa vikundi ambavyo havijarejeshwa
	Mradi wa bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalum kwediboma S/M una changamoto kwenye manunuzi	80,000,000.00	Hakuna uzingatiaji wa Taratibu za Manunuzi katika baadhi ya hatua za Utekelezaji wa Mradi huu.	Jalada ula Uchunguzi limefunguliwa na Uchunguzi umeanzishwa.
Muheza	Mikopo ya 10% za makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa makundi maalum	48,100,000/=	Kiasi cha TSh.40,000,000.00 hazijarejeshwa Kutokana na Udanganyifu	Jalada ula Uchunguzi limefunguliwa na Uchunguzi umeanzishwa.
Pangani	Ujenzi wa Shule ya Sekondari Jumaa Aweso	460,000,000.00	-Ukiukwaji wa Taratibu za manunuzi -Nyufa kwenye Kuta na Sakafu	Mamlaka husika zimetaarifiwa kwa ajili ya kufanya

			-Kutokamilika kwa Mradi husika	marekebisho.
	Ujenzi wa Jengo la OPD katika Zahanati ya Kijiji cha Kimanga	50,000,000.00	Ukiukwaji wa Taratibu za manunuzi	Elimu Kuhusu Taratibu za Manunuzi zimetolewa kwa Wasimamizi na Wajumbe wa Kamati
	Ujenzi wa Chuo cha VETA Pangani	2,811,547,822.49	Tiles zilizoweka ni Tofauti na BOQ	Mamlaka husika zimetaarifiwa kwa ajili ya kufanya marekebisho.
Tanga	Mikopo ya 10% za makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa makundi maalum	1,729,035,729.00	Hakuna Marejesho ya fedha toka kwenye Vikundi vingi vilivyonufaika na mikopo hiyo	Vikundi nufaika vinafuatilwa.
Lushoto	Shule ya Msingi Kwemashait	25,000,000/=	Frem za Madirisha hazikufitishwa vizuri na zipo loose	Ushauri wa Marekebisho umetolewa.
	Mradi wa Ujenzi wa Shule Shikizi Zaghati	250,000,000.00	Matanki yakuhifadhia maji yalipasuka	Ushauri wa Marekebisho umetolewa.
	Mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Bumbuli jengo la maabara	500,000,000.00	Vipimo vya madirisha havikuzingatia BOQ	Ushauri wa Marekebisho umetolewa.

	na OPD			
	Mradi wa ujenzi wa vyanzo vya maji Funta & Irente	578,175,639.00	Mfumo wa kutibu maji haufanyi kazi na chemba bado hazina mifuniko	Ushauri wa Marekebisho umetolewa.
	Mradi wa Ujenzi wa Kituo Cha Afya Cha Kihistoria Kwemakame	50,935,000.00	Mradi umetekelezwa bila kuepo kwa BOQ	Ushauri wa Marekebisho umetolewa.
Jumla		**10,044,396,276.86**		

3. UCHAMBUZI

Ndugu wanahabari,

Katika Uzuiaji Rushwa, Tumetekeleza pia matakwa ya Kifungu cha 7 (a) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329, marejeo ya mwaka 2022, kwa kufanya **uchambuzi wa mifumo** ili kupata tija ya mifumo imara isiyokwamisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Katika hili, TAKUKURU tumafanya uzuiaji rushwa kwa njia ya Uchambuzi wa Mifumo kama inavyoonekana kwenye Jedwali hapo chini.

Jedwali Na. 2: uchambuzi wa mifumo, Lengo Lake, yaliyobainika na pamoja na makubaliano yaliyofikiwa.

mifumo iliyofanyiwa chambuzi	***lengo la Uchambuzi***	***Yaliyobainika katika Uchambuzi***	***Makubaliano katika Warsha***
uchambuzi wa mfumo wa uzingativu wa risiti za EFD na kodi ya zuio katika manunuzi ya vifaa na huduma katika Jiji la Tanga	-Kubaini mianya ya rushwa katika utoaji wa risiti za EFD kwa Halmashauri katika manunuzi ya huduma na vifaa -Kubaini mianya ya rushwa katika ukataji wa kodi ya zuio kwa huduma na vifaa iliyotolewa kwa Halmashauri	-Baadhi ya manunuzi ya huduma na vifaa kutokuwa na risiti za EFD -Baadhi y manunuzi ya huduma na vifaa kutokatwa kodi ya zuio -Baadhi ya kodi ya zuio inayokatwa haiwasilishwi TRA - Wazabuni waliyoko mbali wakishalipwa hawaleti Risiti Mabadiliko ya mfumo wa ulipaji kodi ya zuio kipindi cha Januari 2023 imesababisha wahusika kushindwa kuwasilisha TRA kodi waliyokata	Warsha bado haijafanyika

Uchambuzi wa mfumo Jumuiya za watumiaji maji (CBWSO'S) Handeni	-Kutathmini mfumo wa uendeshaji na ukusanyaji wa mapato kupitia Jumuiya za Usimamizi wa Huduma za Maji Ngazi ya Jamii.	-Mfumo wa ukusanyaji mpato ni mbovu - Kutumia fedha kabla ya kuingizwa kwenye akaunti ya benk. -Ukosefu wa Elimu ya uendeshaji Mradi	- Usimamizi wa ukusanyaji mapato uboreshwe. -Fedha zipelekwe benk kabla ya matumizi na itolewe kwa utaratibu husika -Ofisi za RUWASA wazitembelee Jumuiya na kuwapatia elimu
Ukusanyaji wa mapato ya halmashauri kwa njia ya point of sale (POS)	Kutathmini ya mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri kwa njia ya POS -Kutathmini uwasilishaji wa makusanyo benki ya ushuru na kodi mbalimbali zilizokusanywa katika vyanzo tofauti vya mapato vya Halmashauri. -Kubaini mianya ya	-Kutokuwasilishwa fedha benki kwa wakati - watendaji wa kata na watumishi wengine ambao wamekabidhiwa mashine za POS hawana elimu ya kutosha kuhusiana na mashine hizo - Bill ya malipo (control namba) kutolewa mara moja kwa wiki hii inaleta mianya ya rushwa -	Warsha bado haijafanyika

	rushwa na upotevu wa mapato		
Uchambuzi wa mfumo wa matumizi ya force accout katika miradi ya maendeleo.	Kutathmini majukumu ya kila kamati kama yanafuatwa.	-wajumbe wengi wa kamati hizi hawana elimu ya usimamizi wa miradi -Kazi ya manunuzi kufanywa na mtu mmoja bila kushirikisha wana kamati wenzake -Hakuna utunzaji mzuri wa taarifa za miradi katika ujenzi/ukarabati kama mwongozo wa force account unavyoelekeza. Ukosefu wa fedha/fungu za usimamizi wa mradi ni changamoto kwa wasimamizi wa miradi -Wahandisi kutotembelea miradi mara kwa mara kwa ajili ya kutoa ushauri. Wananchi hawashirikishwi	. Elimu zaidi itolewe kwa Kamati zote zinazosimamia miradi husika. . Wahandisi wahusika wakumbushwe majukumu yao na umuhimu wao katika kusimamia na kutoa ushauri wa kitaalamu katika miradi husika.

		kwenye kuibua miradi	
Uchambuzi wa mfumo wa uendeshaji wa Masoko ya biashara	Kufanya tathmini ya mfumo wa uendeshaji wa masoko ya biashara	- Wilaya ya Mkinga haina sheria ndogo ya Masoko, Gulio na Minada -Baadhi ya Wafanyabiashara kukaidi kulipa ushuru - Wilaya ya Kilindi haina soko la kudumu ila kuna masoko ya kuhama hama(minada) Halmashauri haina umiliki rasmi kwenye maeneo ya masoko hivyo hakuna pango la upangaji katika masoko -Kutokuwepo kwa rejesta ya wafanyabiashara katika soko. -Ukusanyaji ushuru kwa kuandika kwenye daftari bila ya kutoa risiti. -Kukosekana kwa taarifa ya mapato na matumizi. -Fedha zinazokusanywa hazipelekwi benki.	Sheria ndogo ya masoko iandaliwe -Ufuatiliaji kwa wakaiidi ufanyike -Kuwepo kwa rejesta ya wafanyabiashara wote. -Makusanyo yote yatolewe risiti. -Taarifa ya mapato na matumizi iandaliwe kila mwezi. -Kuhakikisha fedha zote zinazokusanywa zinapelekwa benki kabla ya kutumika

Uchambuzi wa mfumo wa utendaji kazi wa Asasi za kiraia	Udhibiti mianya ya rushwa katika utendaji wa Asasi za kiraia	-Kutozingatia kwa kanuni zinazoongoza ufanyaji kazi wa AZAKI. -Ajira kutolewa kwa misingi ya undugu. -Matumizi binafsi ya mali za AZAKI -Usimamizi mbovu wa fedha za AZAKI	-Kuhakikisha kanuni na miongozo ya utendaji wa AZAKI inafuatwa. -Kuhakikisha taratibu za ajira zinafuatwa -Kuhakikisha matumizi sahihi ya mali za AZAKI -Kuhakikisha fedha za AZAKI zinatumika kwa mujibu wa sheria za nchi.
Uchambuzi wa mfumo wa uvunaji na usafirishaji wa mazao ya Msitu	Kutathmini mianya na athari za rushwa katika usimamizi wa mazao ya Misitu	-Ukamataji wa wasafirishaji mazao bila kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa -Kutokuwepo kwa mikataba kati ya wakusanya ushuru na mawakala. -Watendaji, watumishi na wakusanya ushuru kutokuwa na taaluma na elimu zaidi kuhusu mashine za POS na ukusanyaji wa ushuru. -Mawakala kutokuwa na utambulisho	Kufanyika ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maeneo yote yanayotoa huduma - TFS itengeneza utaratibu wa kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara

4. UELIMISHAJI

Ndugu Waandishi wa Habari,

Kifungu cha 7 (b) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329, Marejeo ya 2022, kinaitaka TAKUKURU kuhimiza na kuendeleza uungwaji mkono wa jamii katika kupambana na vitendo vya Rushwa. Sisi tunatekeleza jukumu hili kwa kuelimisha na kushirikisha wadau na umma kwa ujumla katika mapambano dhidi ya rushwa.

Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/2023, TAKUKURU Mkoa wa Tanga imefanya jumla kazi mbalimbali kama inavyooneka katika jedwali hapo chini.

Jedwali Na. 3: Utekelezaji Kazi za Elimu kwa Umma.

Semina	Kufungua Klabu	Uimarishaji Klabu	Maonesho	Vipindi Vya Redio Na T V	Utoaji Wa Habari	Mkutano Wa Hadhara
52	2	128	10	23	17	50

Aidha katika Utekelezaji wa Jukumu hili, tumewafikia wananchi wapatao 87200 kwa njia ya Mikutano ya Hadhara na Maonesho, wanafunzi wa Shule na Vyuo wanaofikia 7400 kupitia Klabu za Wapinga Rushwa, pamoja na makundi mbalimbali ya wadau watoa huduma ambao ni watumishi wa umma, watumishi sekta binafsi pamoja na wale waliojiari katika fani mbalimbali zinazohusika na huduma kwa jamii na idadi yao ni kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini:

Jedwali Na. 4: Makundi yaliyofikiwa katika Utekelezaji Uelimishaji.

Sekta	Me	Ke	Jumla
Utawala	2278	2405	4683
Usafirishaji	200	123	323
Umeme	235	119	354
Ulinzi	300	34	334

Ujenzi	27	19	46
Maji	75	67	142
Huduma za Jamii	2144	305	2449
Fedha	144	102	246
Elimu	22899	25101	48000
Biashara	8	24	32
Afya	103	78	181
Jumla	28413	28377	56790

5. TAKUKURU RAFIKI

Ndugu Waandishi wa Habari,

katika kuongeza wigo wa Ushiriki wa Wadau katika Mapambano dhidi ya Rushwa nchini, TAKUKURU imezindua program ya TAKUKURU-Rafiki kwa la kushirikiana na wadau kutatua kero ambazo zikiachwa zinaweza kusababisha vitendo vya rushwa. Tunatekeleza Programu hii kwa Kufika kwa wadau wanufaika wa huduma na kufanya Utambuzi na Uchambuzi wa Kero kwa njia ya Mikutano ya Hadhara ngazi ya Kata na kisha kuziwasilisha kero hizo kwa wadau watoa huduma ili wazitambue na wazitafutie ufumbuzi au suluhisho ambalo wanakuja kuliwasilisha katika Kujadili Utajuzi wa kero ambapo majibu yake ndiyo mrejesho unaorudishwa kwa wadau wanufaika wa huduma walioibua kero ile. Lifuatalo ni ***Jedwali kuonesha kero zilizotambuliwa kwa kuonesha Sekta husika, Hatua zilizochukuliwa; Vikao na Wanufaika na Vikao na Watoa Huduma katika sekta zilizogushwa na program hii katika mkoa wa Tanga;***

Jedwali Na. 5: Utekelezaji wa Takukuru Rafiki kwa Kipindi cha Januari hadi Machi 2023.

Mkoa	Idadi ya Kata Zilizofikiwa	Idadi ya Kero Zilizotolewa	Idadi ya Kero Zilizotatuliwa	Mifano ya Kero Zilizotatuliwa (Sekta)	Mafanikio Katika Mkoa
Tanga	18	233	85	KERO: Kutokukamilika kwa mradi wa maji, kwamba, mabomba yamewekwa lakini maji hayatoki. (Maji) UTATUZI: Wananchi waliarifiwa, kwamba mabomba hayo ni sehemu ya utekelezaji wa miradi mipya ya usambazaji maji na inakamilishwa awamu na ifikapo Juni 2023 maeneo yote yaliyolengwa na mradi yatapata huduma ya maji. KERO: Barabara kutengenezwa chini ya kiwango. Vifusi havina viwango, karavati chache, mifereji ya maji hakuna. (Miundombinu - Barabara). UTATUZI Miradi inayolalamikiwa inatengenezwa inatekelezwa na Mkandarasi ambaye alisimama kwa muda Kutokana na hali ya hewa kutokuwa rafiki kwa Mradi. Ujenzi Unaendelea baada ya mvua	-Wananchi/ wadau wameonesha mwitikio mkubwa katika kushiriki kuibua kero zilizopo kwenye maeneo yao na wawakilishi wamehudhuria vitako vyote vya kujadili utatuzi wa kero. -Kero nyingi zinatatuliwa baada ya kuibuliwa na tunapokea taarifa ya kutatuliwa kero hiyo wakati wa kikao cha Kujadili Utatuzi. -Kuongezeka Idadi ya Maunganisho mapya ya maji Katika Kata ya Pongwe. -Kukamilikwa Miradi ya Umeme katika Mitaa ya Kata ya Pongwe. -Kuwakutanisha Watoa Huduma na Wateja wao

				kupungua. KERO: Wanafunzi kutembea umbali Mrefu toka Kakindu kufuata Huduma ya Elimu (Elimu). UTATUZI: Uhasishaji unafanyika kwa Wananchi kwa Kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Tanga ili kujenga Shule Shikizi ili kupunguzia adha kwa watoto wa darasa la I-III kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya Elimu. KERO:Miradi wa Umeme kutokamilika kwa wakati na katika Mtaa wa Oysterbay-Pongwe (Nishati-Umeme). UTATUZI: Miradi ilisimama Kutokana na Ukosefu wa Vifaa hususani Mashine Umba, ambapo Mchakato wa Manunuzi Unaendelea Tanessco Makao Makuu na kufikia June 2023 miradi hiyo itakamilika. KERO: Uhaba wa Walimu wa Hisabati, katika Shule ya Sekondari Pongwe, unaopelekea wanafunzi kufanya	ambapo masuala kadhaa yahusuyo taratibu na mienendo ya huduma yametolewa.

				vibaya katika mitihani ya somo hilo (Elimu). UTATUZI: Halmashauri ya Jiji la Tanga ilikiri kulitambua tatizo hilo na kwamba miongozi mwa Maombi ya kuletewa watumishi wapya ni pamoja na walimu wa Somo la Hisabati na Masomo ya Sayansi. Wananchi pia walihamasishwa Kushirikiana na Bodi ya Shule Kutafuta Walimu wa Muda wasaidie Ufundishaji wa somo hilo. KERO: Majibu mabaya yasiyo na Staha, yanayotolewa na Baadhi ya Wahudumu kwa Wagonjwa katika Kituo cha Afya Pongwe (Afya). UTATUZI: Uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga, uliipokea kero hiyo na kuweka mpango wa kukaa na wahudumu kuwakumbusha utaratibu na maadili ya utendaji kazi pia kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi watakaosababisha kero hiyo kujirudia KERO: Kukatikakatika kwa Umeme bila ya taarifa kutolewa hali inayopelekea bidhaa za biashara	

				kuharibika na vifaa vinavyotumia Umeme kuharibika (Nishati-Umeme). UTATUZI: Wananchi waliarifiwa na Mamlaka husika kwamba, kukatika kwa Umeme kunatokana na sababu mbalimbali zikiwemo ukarabati na uimarishaji Miundombinu. Mamlaka iliomba radhi kwa wananchi na kuahidi kutoa taarifa kwa makatizo ya Umeme ambayo sio ya dharula.	

6. UCHUNGUZI

Kazi za Uchunguzi.

Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329 Marejeo ya Mwaka 2022, inaitaka TAKUKURU kupokea taaria, tuhuma au malalamiko kuhusiana na vitendo vya rushwa kutoka kwa wananchi na vyanzo vingine. Katika jukumu la kupokea taarifa au malalamiko na Kuchunguza tuhuma au makosa ya Rushwa pamoja na njama za kutendeka kwa makosa hayo, TAKUKURU Mkoa wa Tanga tumefanya kazi ya kupokea malalamiko, yaliyohusisha Sekta mbalimbali, ambapo kuna malalamiko yanayohusu Rushwa na Yasiyohusu Rushwa, tumechukuwa Hatua mbalimbali na kufikia hatua tofauti mpaka sasa kama inavyosomeka kwenye jedwali hapoo chini;

Jedwali Na. 6: Malalamiko, Sekta na Hatua zilizochukilwa na kufikiwa.

Idadi ya malalamiko	Sekta zilizohusika				Malalamiko Yanayohusu Rushwa	Malalamiko Yasiyohusu Rushwa	Hatua zilizochukuliwa na kufikiwa mpaka sasa.
	Sekta		Idadi ya Malalamiko	Kiwango (%)			
162	Tamisemi	Serikali za Mitaa (WEOs, VEOs, MEOs, Ofisi za HROs na DEDs.	54	33.3	81 (50%)	81(50%)	Taarifa 70 zimefungwa.
							Taarifa 11 zimehamishiwa idara zingine.
		Afya	08	4.9			Taarifa 81 zinaendelea Kuchunguzwa
		Elimu	20	12.3			
		Ardhi	23	14.2			
	Mahakama		08	4.9			
	Sekta Binafsi		13	8			
	Majeshi ya Ulinzi na Usalama		11	6.8			
	Mashirika ya Umma		01	0.6			
	Misitu		03	1.8			
	Mazingira		01	0.6			
	Mali Asili		02	1.2			
	Mabaraza ya Ardhi		02	1.2			
	Utalii		01	0.6			
	Nishati		03	1.8			

	Maji	03	1.8			
	Kazi	01	0.6			
	Tasaf	01	0.6			
	Ujenzi	03	1.8			
	Wakala wa Serikali	01	0.6			
	Hifadhi ya Jamii	01	0.6			
	Kilimo	01	0.6			
	Ukusanyaji Mapato	01	0.6			

Ndugu waandishi wa habari,

Jedwali la Malalamiko, Sekta na Hatua zilizochukilwa na kufikiwa, linaonesha kiwango cha malalamiko yasiyohusu rushwa kwenye jedwali hapo juu ni 50% ambayo ni zaidi ya 30%. Hii ina maanisha kwamba, Wananchi wana imani na utendaji kazi wa TAKUKURU kwamba, kwa elimu waliyonayo, wanapoona jambo lolote lililo kinyume na sheria basi kimbilio lao ni Ofisi ya TAKUKURU, na sisi tumekuwa tukiwakipokea wateja wetu japo malalamiko yao si ya vitendo vya rushwa na tunatumia fursa ya ujio wao kuwaelimisha Kuhusu tofauti kati ya makosa ya rushwa na masuala mengine yaliyo kinyume na sheria ambayo sio makosa ya rushwa na kisha tunawashauri namna ya kutatua au kushughulikia malalamiko yao kwa utaratibu ulio bora na sahihi kwa mujibu wa Sheria.

7. MASHTAKA.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Kwa ujumla Katika Kupambana na Vitendo vya Rushwa kupitia Utekelezaji wa Jukumu hili, tumefanya kazi kwa Kufungua Mashauri Mahakamani, ambapo yapo mashauri ambayo katika Maamuzi, mahakamani mahakama imetupa ushindi kwa maana ya kuwatia hatiani watu humiwa kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini:

Jedwali Na. 7: Idadi ya Mashauri na Maamuzi Mahakamani

Idadi ya Mashauri mapya	Idadi ya Mashauri yanayoendelea Mahakamani	Idadi ya Mashauri yalifanyiwa Maamuzi mahakamani	Idadi ya maamuzi ambayo Jamhuri ilishinda	Idadi ya maamuzi ambayo Jamhuri ilishindwa
5	27	3	2	1

8. USHIRIKIANO NA WADAU

Ushirikiano na wadau.

Kifungu cha 7 (b) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 Marejeo ya Mwaka 2022, kinaitaka TAKUKURU kuhimiza na kuendeleza uungwaji mkono wa jamii katika kupambana na vitendo vya Rushwa. Sisi tunatekeleza jukumu hili kwa kuelimisha na kushirikisha wadau na umma

kwa ujumla katika mapambano dhidi ya rushwa. Lifuatalo ni Jedwali kuonesha wadau ulioshirikiana nao pamoja na maeneo ya ushirikiano;

Jedwali Na. 8: Ushirikiano na Wadau

Jina la Mdau tuliyeshirikiana naye	***Eneo la Ushirikiano***	***Mafanikio Kutokana na Ushirikiano huo***
Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi na Huduma (Veta) Tanga	Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu 2022	Kongomano la Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu 2022
Waandishi wa Habari na Vyombo vya Habari	Utoaji Taarifa kwa Umma.	Kufikisha Taarifa 3 kwa Umma Kuhusiana na Utendaji Kazi wa TAKUKURU kwa kila Robo Mwaka.
Vyombo vya Habari	Uelimishaji na Elimu kwa Umma kwa njia	Uelimishaji na Utoaji Elimu kwa Umma
Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS)	Maoni ya Kisheria na Utoaji Vibali vya Kufungua Mashauri ya Rushwa na Uhujumu Uchumi Mahakamani	Ufunguaji na Uendeshaji wa Mashauri ya Rushwa na Uhujumu Uchumi Mahakamani
Skauti	TAKUSKA	Uelimishaji wa Uhamasishaji Vijana Kuhusu Uzuiaji Vitendo vya Rushwa.

9. MAADHIMISHO YA WIKI YA SHERIA

Ndugu wandishi wa Habari, TAKUKURU pia ni wadau katika maadhisho ya wiki ya Sheria na siku ya Sheria. Kwa mwaka huu 2023, Takukuru Mkoa wa Tanga tumeshirikiana na Mahakama pamoja na wadau wengine katika maadhimisho ya wiki ya Sheria na siku ya Sheria. Lifuatalo jedwali linaloonesha shughuli tuliyoifanya na wadau tulioshirikiana nao;

Jedwali Na. 9: Maadhimisho ya Wiki ya Sheria

Shughuli iliyofanyika	***Jina la Mdau tuliyeshirikiana***

	naye
Vipindi 4 Redio na Kipindi 01 cha Televisheni	Mahakama, TLS, TAWLA, Jeshi la Polisi, Idara ya Huduma za Uangalizi, Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya.
Uelimishaji kwa njia ya Onesho la Maadhimisho ya Wiki ya Sheria	Mahakama, TLS, TAWLA, Jeshi la Polisi, Idara ya Huduma za Uangalizi, Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya.
Kutembelea magereza na kufanya uelimishaji kwa Wafungwa	Mahakama, TLS, TAWLA, Jeshi la Polisi, Idara ya Huduma za Uangalizi, Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya.
Kutembelea Shule za Msingi na Sekondari na Kuelimisha Wanafunzi na Walimu	Mahakama, TLS, TAWLA, Jeshi la Polisi, Idara ya Huduma za Uangalizi, Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya.
Kushiriki katika Maandamano ya Ufunguzi/Uzinduzi wa Wiki ya Sheria	Wananchi, Klabu za Jogging, Mahakama, TLS, TAWLA, Jeshi la Polisi, Idara ya Huduma za Uangalizi, Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya.

10. MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

Ndugu wandishi wa Habari, TAKUKURU kama sehemu ya jamii, hatukuwa nyuma na wala hatukujitenga katika maadhisho ya Siku ya Wanawake. Kwa mwaka huu 2023, Takukuru Mkoa wa Tanga tumeshirikiana na wadau wengine katika maadhimisho hayo. Lifuatalo jedwali linaloonesha shughuli tuliyoifanya na wadau tulioshirikiana nao

Jedwali Na. 10: Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

shughuli iliyofanyika	***Jina la Mdau tuliyeshirikiana naye***
Onesho la Maadhimisho ya Wiki ya Sheria	Benki za CRDB, NMB, Jeshi la Polisi, Wajasiriamali, Tree of Hope, Halmashauri ya Jiji la Tanga, World Vision, Klabu ya Wapinga Shule ya Sekondari Mkwakwani.

11. MIKAKATI YA APRILI -JUNI 2023.

Ndugu wanahabari,

Katika kutekeleza Majukumu yetu yote matatu kwa maana ya Uchunguzi, Elimu na Uzuiaji Rushwa, tutajikita Zaidi katika maeneo yafuatayo:

Kwanza, Katika Ushirikishaji wadau, tunaendelea kutekeleza Programu ya TAKUKURU Rafiki, kwa kuzifikia kata nyingi zaidi ili kuongeza ushiriki wa kila mwananchi na wadau katika kukabili tatizo la rushwa katika Utoaji huduma kwa jamii na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Tutaendelea kufanya vikao vya utambuzi na uchambuzi wa kero katika ngazi ya kata hususani katika masuala ya Utoaji na upokeji huduma kama za afya au elimu pamoja na mchakato wa kutekeleza miradi ya maendeleo. Utatuzi wa kero hizo ni hatua madhubuti za udhibiti na uzuiaji rushwa kwa sababu zikiachwa pasipo kutatuliwa au kupatiwa ufumbuzi zinaweza kusababisha kutokea kwa vitendo vya rushwa.

Kwa nafasi ya kipekee, nitoe shukrani za dhati kwa Wadau Wadau Watoa huduma hususani Wakurugenzi wa Halmashauri zote za Mkoa wa Tanga, TANESCO, Tangauwasa na Mashirika na idara zingine za Serikali na kwa ushirikiano waliotupa kwani, Baada ya kutambua kero hizo, tumeziwasilishwa kwao, wamezitafutia ufumbuzi na tumefanya vikao vya kujadili Utatuzi wa kero kwa kushirikisha wananchi, viongozi wa kisiasa, watendaji wa Serikali na wazabuni, na kwa pamoja tumetatua kero hizo au kuweka mikakati ya jinsi ya kuzitatua kwa pamoja. Tumetekeleza mikakati tuliyoweka, ikiwamo Kutoa mrejesho kwa umma juu ya utatuzi wa kero zilizoibuliwa na kutatuliwa ili kufikia malengo ya Programu hii.

Pili, sambamba na TAKUKURU Rafiki, tunaendelea kutoa Elimu ya Mapambano dhidi ya Rushwa kwa kuyafikia Makundi mbalimbali kiidara na katika jamii. Katika hili tumepanga kukutana na Kamati mbalimbali zinazohusika na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Force Account, Walimu Walezi wa Klabu za Wapinga Rushwa na pia kuwakutanisha wadau wenye jukumu la utoaji huduma kwa lengo la kuufahamisha umma juu ya namna bora ya kushirikiana katika kufanikisha azma ya serikali katika kuwahudumia wananachi. Sambamba na hilo tutajielekeza pia kwenye Ufuatiliaji wa Miradi ya Ujenzi katika Wilaya zote za Mkoa wa Tanga hususani Ujenzi wa Miundombinu ya Shule za Msingi kupitia Mradi wa Boost kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo Mkoa wa Tanga umepatiwa Jumla ya **Shilingi 11,442,000,000/=.** Lengo letu ni Kuhakikisha kwamba fedha zinazotolewa na serikali zinatumika kukamilisha

miradi husika kwa wakati na kwa ubora unaolingana na thamani ya fedha iliyotengwa na kutumika. Ninawakumbusha wasimamizi wa miradi ya maendeleo kuzingatia uadilifu na uaminifu katika utekelezaji majukumu yao sambamba na uzingativu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayotolewa kwa mujibu wa sheria. Nawakumbusha tu, Popote Walipo TAKUKURU ipo na hatutasita kuchukua hatua za Kisheria dhidi wale wote watakaofanya ubadhilifu, ufujaji au njama zozote za kuhujumu fedha zilizotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Tatu, tumejipanga na tunaendelea na uzuiaji Rushwa katika Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali na kipekee, tunaendelea kufanya Utambuzi wa vyanzo vyote vya Mapato ya Halmashauri zote kwa kupitia Bajeti za Halmashauri hizo na kufuatilia mifumo ya ukusanyaji mapato kwa njia ya kielektroniki (POS) ili kuweka udhibiti Madhubuti kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ukusanyaji mapato. Tutafuatilia pia uzingatiaji sheria katika Kufanya Makato ya Kodi ya Zuio wakati wa Kulipia bidhaa au Huduma. Ninawakumbusha Maafisa Masuuli na wadau wote wenye jukumu la kusimamia na kutoa taarifa Matumizi ya fedha katika taasisi zao, kutekeleza kwa ufasaha jukumu la Ukusanyaji wa Kodi ya zuio kutekeleza wanapolipia bidhaa au huduma na Kuwasilisha makato hayo kwenye Mamlaka ya Mapato Tanzani (TRA) kwa wakati au mapema iwezekavyo.

Nne, Katika Ufuatiliaji wa Matumizi ya Rasilimali za Umma, tumejipanga kufuatilia Uzingatiaji Sheria, taratibu na kanuni katika Matumizi ya Fedha za Serikali na kwa umuhimu wa kipekee, tutapitia Taarifa mbalimbali za Ukaguzi wa ndani na nje ili kubaini na kufuatilia kwa undani hoja za Ukaguzi na majibu yanayotolewa kama yanakidhi lengo la Uwajibikaji na Uadilifu katika Matumizi ya Rasilimali hizo.

12. HITIMISHO

Ndugu zangu wanahabari,

Naomba nihitimishe kwa kutoa rai kuwahamasisha wakazi wa Mkoa wa Tanga na wadau wote kwa ujumla kupitia ninyi waandishi wa Habari, kwamba waendelee kutupa ushirikiano wakati wote, hususani kupitia Programu ya TAKUKURU-Rafiki, ambayo inalenga kuongeza ukaribu baina ya TAKUKURU, wananchi na wadau ili, kwa namna rafiki, tushirikiane kuzuia vitendo vya rushwa visitokee katika Utoaji wa huduma kwa umma na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Tuzingatie pia Kifungu cha 39 (1) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11/2007, kwamba kila mwenye taarifa juu ya vitendo vya rushwa, atoe taarifa TAKUKURU.

Tunaomba pia Ushirikiano wenu Mahakamani pale mtakapohitajika Kutoa ushahidi mahakamani ili tukamilishe mchakato wa haki jinai katika Mapambano dhidi ya rushwa.

Kwa Taarifa za vitendo vya rushwa, Karibuni katika Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Tanga iliyopo BOMBO AREA karibu na HARBOURS CLUB na kwa wale waishio wilayani wasisite kufika katika ofisi za TAKUKURU zilizopo katika Wilaya husika. Vinginevyo, Unaweza kutumia Huduma ya BURE kwa kutupigia simu ya dharura namba 113 au kutuma ujumbe mfupi wa maandishi kwa kupiga *113# na kisha kufuata maelekezo, ili kututaarifu juu mtu yeyote anayekiuka sheria na kufanya uhalifu kwa kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Wito wangu kwa kila mwananchi anayenisikiliza au kusoma habari hii, ni kwamba usikae pembeni katika uzuiaji vitendo vya rushwa, bali tushirikiane ili kwa pamoja tuweze kuimarisha udhibiti wa vitendo vya rushwa. Tutekeleze wajibu tuliopewa na ibara ya 27(1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, wajibu wa kulinda rasilimali za umma na Kupiga vita aina zote za ubadhilifu na kuendesha Uchumi wa taifa kwa umakini kama watu ambao ni waamuziwa hatma ya taifa letu. Una Wajibu wa kufuatilia uzingativu wa sheria na uadilifu hususani katika Matumizi ya rasilimali za umma. Ufuatiliaji wako si lazima uwe wa kitaalamu bali ni ukaribu na udadisi wa kufahamu kila kinachoendelea katika miradi kwa lengo la kujua endapo fedha zinazotolewa na Serikali zinatumika kama ilivyokusudiwa

Ndugu Waandishi wa Habari,

Kauli mbiu inayotuongoza kwa sasa katika udhibiti na uzuiaji vitendo vya rushwa ni **"KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU: TUTIMIZE WAJIBU WETU".**

Imetolewa na:

Mariam Mayaya

***Kny:* KAIMU MKUU WA TAKUKURU (M)**

TANGA

Simu 0738 – 150225